



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA



Barua zote zitumwe kwa:

Simu: +255 27 2548072/2503494 (Director)

+255 27 2544330 (General)

Nukushi: +255 27 2545768

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.AB.156/423/01/11

Mkurugenzi wa Jiji

S. L. P. 3013,

20 Barabara ya Boma,

23101 ARUSHA,

Barua Pepe: cd@arushacc.go.tz

Tovuti: www.arushacc.go.tz

Tarehe: 13 Desemba, 2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA (AJIRA YA MUDA MAALUMU)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Jiji la Arusha kutuma maombi ya kazi ya muda kwa Mkurugenzi wa Jiji kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Nafasi hizi ni za muda wa miezi mitatu kwa kazi zilizopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022


SN	KADA/KAZI	IDADI YA NAFASI	SIFA ZINAZOTAKIWA
1	Dereva II(magari)	5	Mwombaji awe na Elimu ya kidato cha nne na Leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi(VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali Mshahara: - Utalipwa katika ngazi ya TGS B1
Kazi na Majukumu ya Dereva II j) Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali na usalama wa gari k) Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari l) Kufanya usafi wa gari m) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali			

MAELEZO YA JUMLA

- a. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na Mwenye akili timamu
- b. Waombaji wawe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- c. Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, cheti cha kuzaliwa na maelezo binafsi (CV)
- d. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/12/2021 saa 9:30 alasiri
- e. Waombaji wenye uzoefu wa kazi watapewa kipaumbele
- f. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji la Arusha
S.L.P. 3013,
Arusha.

Tangazo hili limetolewa na:



John M. Pima (Ph.D)
**MKURUGENZI WA JIJI
ARUSHA**

**MKURUGENZI WA JIJI
JIJI LA ARUSHA**